

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



25 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA – TAREHE 25 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**294. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA
CHRISTOPHER MNZAVA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itazirejesha Fedha za ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Msalala zilizorudishwa na mfumo baada ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 kuisha.

295. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILI ZODO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kada ya Elimu inakadiriwa kuwa na upungufu wa Walimu takriban 60,000:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kukabiliana na changamoto hiyo.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

296. MHESHIMIWA MAIDA HAMADI ABDALLAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Baadhi ya Vijiji vilivyoorodheshwa kwa ajili ya kufikiwa na Mradi wa TASAF II kwa upande wa Zanzibar bado havijafikiwa na Mradi unaelekea mwisho:-

Je, Serikali inasemaje juu ya maeneo hayo ambayo hayajafikiwa na Mradi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**297. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO
NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ya Kilolo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**298. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMMED
ISSA (MTAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali italetwa Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Mkopo wa Elimu ya Juu ili kuwapunguzia mzigo mkubwa wa malipo wanufaika wa mkopo huo.

**299. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itatoa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Watu wenye Ulemavu kama ruzuku badala ya mikopo kama ilivyo sasa.

WIZARA YA NISHATI:

300. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTI (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati: Je, ni lini Serikali itawalipa fidia ya kupisha njia kubwa ya umeme Wananchi wa Vijiji vya Lengijape, Ilkurot na Olkejulenderit katika Jimbo la Arumeru Magharibi.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

301. MHESHIMIWA AHMED YAHYA ABDULWAKIL (KWAHANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Shirika la Posta Zanzibar halioni umuhimu wa kuchimba kisima katika Jimbo la Kwahani katika Kitongoji kilichopo karibu na Ofisi hiyo ili kukuza ujirani mwema.

302. MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Mawasiliano ya Simu yenye usikivu katika Kata za Litehu, Ngunja na Mkwiti Wilayani Tandahimba.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

303. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):

• Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo sugu la ujenzi holela Mijini.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

304. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusamehe kodi za miaka ya nyuma Taasisi za Dini

zilizokuwa zikiendeshwa kwa utaratibu usiolenga kupata faida na kuziwekea utaratibu Taasisi hizo kuanza kulipa tangu walipojulishwa kutakiwa kulipa kodi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
25 MEI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**